

**KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO
IDARA YA UCHAPISHAJI UNIONI YA KUSINI NA KASIKAZNI
MWA TANZANIA**

JUMA LA MAOMBI LA ROHO YA UNABII
(JUMA LA URITHI WA KANISA)
10-17/10/2026

**NENO KUU: MUNGU WA MAMBO MAPYA NA
MIANZO YA MATUMAINI**

Limeandaliwa Na

IDARA YA UCHAPISHAJI UNIONI YA KUSINI YA KANISA LA
WAADVENTISTA WA SABATO TANZANIA

YALIYOMO

Utangulizi.....	03
Somo la kwanza: Mungu wa Mambo Mapya.....	04
Somo la pili: Sauti Yenye Tumaini katikati ya dhoruba.....	07
Somo la tatu: Karama ya Unabii katika Agano La Kale.....	12
Somo la nne: Karama ya Unabii katika Agano Jipya.....	18
Somo la tano: Karama ya Roho ya Unabii katika siku za Mwisho.....	22
Somo la sita: Kazi na faida ya kipawa cha Unabii.....	26
Somo la Saba: Ushindi katikati ya Mkanganyiko.....	29
Somo la Nane: Sifa mbili Bainifu.....	33

UTANGULIZI

Kanisa la waadventista wa sabato kila mwaka limekuwa likisherehekea mwezi wa urithi wa kanisa (Adventist Heritage Month) mwezi wa kumi. Msisitizo katika sherehe umekuwa ni kuangalia kule ambako Mungu amelitoa Kanisa Lake, mahali lilipo na kule linakoelekea, huku Mkazo mkuu ukijikita kufanya uamusho wa kiroho kwa njia ya kujifunza maandiko matakatifu.

Urithi wa kiadventista (Adventist Heritage) hujumuisha mambo mengi ikiwemo kutumbusha historia ya kanisa letu, misingi ya Imani yetu, mtindo wa maisha na mchango wa kanisa la waadventista wa sabato katika jamii tangu kuanzishwa kwake katikati ya karne ya kumi na Tisa.

Mambo tunayoweza kuyaangalia na kuyatafakari ni kama ifuatavyo:

1. Katika chimbuko la kihistoria-tunaangalia urithi wa kanisa letu katika agano la kale, agano jipya, na historia ya kanisa lilivyozaliwa baada ya Vuguvugu la ujio wa Yesu Kristo mara ya pili (Millerite Movement) miaka ya 1840 na hata kuanzishwa kwake baada ya kukatishwa tamaa.
2. Katika misingi ya Imani tunaangalia misingi ya mafundisho ya Imani yetu kama vile Ujio wa Yesu, Sabato, utume wetu na kadharika.
3. Katika mtindo wa Maisha tunaangalia mwenendo wetu, ujumbe wetu wa afya, mavazi na tabia.
4. Upande wa michango ya kijamii tunaangalia namna kanisa ambavyo limekuwa likijihusisha na huduma katika Jamii kama vile 1. Elimu-Shule na vyo 2. Afya-hospitali na zahanati zinavyotoa huduma katika jamii 3. Huduma za Kibinadamu kama vile ADRA-shirika linalojihusisha kugusa maisha ya binadamu wakati wa Majanga na Umaskini.

Mwaka huu, Juma au Sabato ya Roho ya Unabii na Urithi wa Kiadventista inatualika washiriki sote kutafakari karama ya kibiblia ya roho ya unabii pamoja na ushawishi wake katika maendeleo, imani, na utume wa Kanisa la Waadventista Wasabato.

Juma hili la Roho ya unabii limeandaliwa katika mkitadha wa Sauti moja ya utume kwa wote: Mambo Yote mapya, Tumaini linaanzia hapa. Jambo hili muhimu linahitaji kila mshiriki kuwa na uelewa kuhusiana na karama ya Unabii kama inavyofundishwa na kanisa la waadventista wa Sabato. Baada ya hatua hiyo wote pia tayari kutekeleza utume wa kanisa wa kuwaadaa watu kwa ajili ya kuja kwa Mfalme na Mwokozi wetu Yesu Kristo hivi karibuni.

Masomo haya yameandaliwa na Union yetu ya kusini mwa Tanzania na Halmshauri kuu ya kanisa la Waadventista wa Sabato ulimwenguni. Tunapenda kuyaalika makanisa yote katika Union yetu na kila mshiriki mmoja mmoja kuweza kushiriki kikamilifu katika juma hili maalumu la Uamusho kupitia Idara ya Roho ya unabii. Mungu awabariki.

Mambo Yote Mapya Tumaini linaanzia Hapa.

Somo la Kwanza

MUNGU WA MAMBO MAPYA

Na Pr. Elias J Misungwi

Mkurugenzi wa Idara ya Uchapishaji na Roho ya unabii

Union ya Kusini mwa Tanzania.

Fungu kuu: **Isaya 43:19-** *“Tazama, nitatenda neno jipya; sasa litachipuka; je! Hamtalijua sasa? Nitafanya njia bata jangwani, na mito ya maji nyikani.”*

Utangulizi: Mungu ni Mungu wa mambo mapya. Mungu anapenda mambo mapya. Maandiko matakatifu yanadhihirisha kabisa kuwa Mungu ndiye chanzo kikuu cha ubunifu, mabadiliko, uumbaji, maarifa na teknolojia inayoendelea kuvumbuliwa siku kwa siku. Mungu daima na siku zote haachi kufanya mambo kuwa mapya na yenye kuleta matumaini.

Nini Maana ya neno Jipya/Mapya- Chadash (חדש).

Isaya 42:9, “Tazama, mambo ya kwanza yamekuwa, nami natangaza mambo yaya; kabla hajayatokea nawapa habari zake.” Katika maandiko matakatifu Mungu anawaambia waisrael kupitia kinywa cha nabii Isaya kuwa Yeye ni Mungu mwenye kufanya mambo yasiyokuwako yakatokea. Maneno “jambo jipya” au “kitu kipya” katika lugha ya Kiebrania yanatokana na neno Chadash (חדש); ambayo yanaonyesha maana mbili:

1. Kipya au Kiasili:

Kitu ambacho hakijawahi kuwepo kabisa au ambacho hakijatokea hapo mwanzo. Hii humaanisha kuwa Mungu ni mwenye wa ajabu na wapekee mno kuliko maelezo yote ya mwanadamu. Huyu ndiye Bwana Mungu wetu. Amen.

Maandiko yanasema kuwa hapo Mwanzo Mungu aliumba Mbingu na Nchi. Kabla ya Mungu kuumba mbingu na nchi hazikuwapo. Kwa kuwa Mungu ni Mungu wa mambo mapya alipoumba na alifanya mambo mapya yakatokea kama tunavyoshuhudia katika kitabu cha Mwanzo 1, na mwanzo 2. Hebu tutafakari utendaji wake katika juma la uumbaji wake:

1. Na Mungu akasema: “Kuwe na nuru.” Basi kukawa na nuru. Mwanzo 1:3
2. Mwanzo 1:6 Kisha Mungu akasema: “Na kuwe na anga, katikati ya maji, na anga liyatenganishe maji na maji.
3. Mwanzo 1:11- Kisha Mungu akasema: “Dunia na ichipushe majani, mimea inayozaa mbegu na miti ya matunda inayozaa matunda kulingana

na aina zake, miti inayozaa matunda yenye mbegu duniani.” Na ikawa hivyo.

4. Mwanzo1: 14- Kisha Mungu akasema: “Na kuwe na mianga katika anga la mbingu ili itenganishe mchana na usiku, nayo itakuwa ishara ya kuonyesha majira na siku na miaka.
5. Mwanzo 1:20- Kisha Mungu akasema: “Maji na yajae viumbe walio hai, na viumbe wanaoruka waruke juu ya dunia katika anga la mbingu.”
6. Mwanzo 1:24- Kisha Mungu akasema: “Dunia na itokeze viumbe walio hai kulingana na aina zao, wanyama wa kufugwa na wanyama wanaotambaa na wanyama wa mwituni kulingana na aina zao.” Na ikawa hivyo.
7. Mwanzo 1:26- Mungu akaanzisha taasisi ya ndoa ukawa mwanzo wa Jamii ya wandamu. Kisha Mungu akasema: “Na tufanye+ mtu kwa mfano+ wetu, kulingana na sura yetu, nao wakatawale samaki wa baharini na viumbe wanaoruka angani na wanyama wa kufugwa na dunia yote na kila mnyama anayetambaa duniani.
8. Mungu akaanzisha Taasisi ya ibaada ya kumwabudu Yeye ili kukumbuka Ukuu wake kuwa Yeye ni Mungu, lakini pia Yeye ni Mungu wa Mambo Mapya.

Mwanzo 2:1-3- “Basi mbingu nan chi zikamalizika, na jeshi lake lote. Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi kazi yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi. yake yote aliyoifanya. Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na kuifanya.”

Hapa tunaona mpango mzima wa juma la uumbaji, utaratibu, na ukamilishwaji wa kazi zote ndani ya juma moja la uumbaji wa mbingu na nchi. Na kazi zote anazifanya kwa Neno Lake lenyewe uweza wa ajabu, isipokuwa katika swala zima la kumuumba mwanadamu. Ulimwengu wetu huu unatokana na Bwana Muumbaji Mwema na wa pekee.

2. Kufanya Upya / Kurejesha:

Maana ya pili ya neno Chadash ni kitendo cha kurudisha au kurejesha kitu au kukifanya upya kiwe na uhai na utukufu mwingine tofauti na cha zamani. Hii inamaanisha kuwa Mungu anao uwezo wa kurejesha upya kitu kilichoharibika, afya iliyoharibika au maisha yaliyoharibika. Yeye ndiye anayewapatia watu uzima wasio na uzima.

Yeye ndiye aliye na uwezo wa kufufua watu waliokufa, yeye ndiye aliye na uwezo wa kubadili miili ya kuharibika na kuivisha kutokuhariba nk.

SIFA ZA KAZI ZA UTENDAJI WAKE

Bwana Mungu siyo Mungu wa mambo Mapya peke yake, bali ni Mungu wa mambo mazuri na yanayopendeza. Mungu alifanya mambo mapya yaliyo mazuri. Kamwe kwake mambo mapya mabaya yasiyopendeza hayawezi kuwa yake.

Mambo mapya ambayo tangu zamani na hata leo anayoyatenda yana sifa zifuatazo: Mwanzo 1:4, 10, 12, 18, Moja: Mema sana, Mbili, Yenye kupendeza, Tatu, Matakatifu/kamilifu –aliumba au mwanadamu mtakatifu/mkamilifu, ndoa takatifu, sabato takatifu nk

Mambo gani tunayofunza kutokana Utendaji wa Mungu?

1. Mungu wetu anao uwezo wa kutubadilisha na kuwa viumbe vipya.
2. Yeye anaweza kubadilisha hali yetu ya maisha duni kuwa nzuri
3. Mungu anaweza kutureshea afya zetu, uchumi wetu, ndoa zetu, mahusiano yetu yaliyoharibika
4. Mungu si Mungu wa mambo ya zamani tu ni Mungu wa mambo ya sasa pia
5. Utendeji kazi wa Mungu si wa kizamani
6. Mungu anataka tutekelezeje Utume alitukabidhi?
7. Mungu anahitaji wafuasi wake watumie mbinu mpya katika kufanya kazi yake ya utume. Mfano: kutoa au kufundisha au kufanya mahubiri kwa njia ya kidijitali kaitka maeneo na kwa namna mbali mbali.

WITO: Hebu turuhusu Bwana afanye jambo jipya katika maisha yetu. Tuombe Bwana aweze kububadilisha maisha yetu ya kiroho, kijamii, Kimwili kiuchumi na kiakili pia. Mungu atusaidie tukubali kutumia Njia mpya na mbinu mpya katika kutekeleza agizo alilotupatia.

Mungu ni Mungu wa Mambo mapya, mbinu mpya zilizo njema, zinazopendeza, na takatifu Hebu Jiweke wakfu ili Mungu akupatie utambuzi wa kiroho ili uweze kutumika kwa ajili ya kazi yake.

Maswali ya kutafakari:

1. Unaitumiaje teknolojia aliyoleta Mungu katika kutatua changamoto zako binafsi
2. Kanisa lako mahalia limepokeaje na linaitikiaje mambo mapya yanayokuja ili kusaidia kumaliza kazi ya Bwana?

MAMBO YA KUOMBEA: Tuombee Roho Mtakatifu maishani. Bila uongozi na nguvu ya Roho Mtakatifu, hatuwezi kuishi maisha ya ushindi wala kumtumikia Mungu ipasavyo. Tunapoomba uwepo wake, tunakaribisha uongozi, faraja, na karama za kiroho katika maisha wetu ya kila siku.

Mhudumu / Kanisa laweza kuongeza mambo mengine ya kuombea katika nafasi hii.

Somo La Pili

SAUTI YENYE TUMAINI KATIKATI YA DHORUBA

Na Elias J Misungwi

Mkurugenziwa Idara ya Uchapishaji na Roho ya Unabii

Union ya kusini mwa Tanzania

Fungu kuu: **Mwanzo 3: 8-9** *Yule mwanaume na mke waliposikia sauti ya Bwana Mwenyezi Mungu akitembea bustanini jioni, wakajificha kutoka kwa Bwana Mwenyezi Mungu katikati ya miti ya bustani. Lakini Bwana Mwenyezi Mungu akamwita Adamu, "Uko wapi?"*

Utangulizi: Mungu mwenyezi alifanya kila kitu kwa uzuri; na vitu vyote vililikuwa vinaonekana vizuri. Hakukuwa na kitu chochote kibaya. Mimea ilikuwa mizuri, wanyama walikuwa wazuri, maji yalikuwa mazuri, hewa ilikuwa nzuri, uoto wa asili ulikuwa mzuri na kila kitu kilichokuwa kimefanywa kilikwa ni chema sana cha chakupendeza.

Mungu alimfanya mwanadamu kwa sura yake na kwa mfano wake. Mwadamu alikuwa mwema, mtakatifu, asiye na dhambi.

Kijamii –mahusiano yao yalikuwa mazuri, walipendana. Kimwili-miili yao ilikuwa inapendeza sana, hakukuwa na magonjwa. Walikuwa na mavazi ya utukufu kama Malaika.

Kiakili- uwezo wao wa kuelewa mambo ulikuwa mkubwa sana. Hawakuhitaji kwenda shule kufundishwa. Ndio maana Adamu alipopewa kazi kuvipatia viumbe ambavyo Bwana Mungu alivyokuwa ameviumba, aliweza kuvipatia viumbe vyote ambavyo Bwana Mungu alivyokuwa ameviumba. Yaani viumbe vya angani, majini na hata viumbe vya ardhini. Adamu hakuhitaji kwenda shule ili kuelewa jinsi ya kutekeleza jambo hili la Bwana Mungu alilokuwa amempatia kulifanya.

Kiutawala- Mwanadamu alipewa kazi ya kutawala na kuvitiisha vitu vyote ambavyo Bwana Mungu alikuwa ameviumba na kuvifanya. Hivyo basi ulimwengu mpya wa viumbe vipya ambao Bwana Mungu alikuwa ameviumba ulikuwa Mpya. Kwa jinsi hii wanadamu kwanza waliishi kwa Amani na furaha wakiwa na mwunganiko, na mahusiano mazuri na Mungu wao aliyekuwa amewaumba.

Bwana Mungu alihitaji viumbe hawa aliowaumba kwa mfano wake na kwa sura yake wadumishe uhusiano wao na Yeye kwa njia kumwabudu na kupumzika siku ya Saba ya juma, na kwamba kwa kufanya hivyo walikuwa wanaonesha kuwa ulimwengu wote pamoja na wao ni mali ya Bwana Muumbaji wao. Uzuri wao na utakatifu wao na umoja wao na utawala wao kwa viumbe vyote, kuishi kwao milele kungewezekana tu kama wangelidumu kubakia katika maneno yaliyotoka katika sauti yake.

MWANZO WA DHORUBA

Maandiko matakatifu yanasema kulikuwa na vita Mbingu. ufunuo 12:7,8,12. Baada ya shetani kuanzisha uasi na vita mbinguni, akashindana na Mungu kwa kutaka kufanana na Mungu, Isaya 14:13-14. Lusifa alikuwa kiumbe mzuri aliyekuwa ameumbwa na Mungu kama maandiko matakatifu yanavyosema katika kitabu cha Ezekili 28:13-15. Maandiko matakatifu yanasema kuwa Lusifa alikuwa ameumbwa kwa utukufu, Kerubi, afunikaye, na alikuwa na uwezo au vipawa na ujuzi mwingi.

SHIDA YAKE KUU ILIKUWA NI NINI? Uzuri alioumbwa nao, dhamana ya utawala na mamlaka aliyokuwa amepewa kuwaongoza wenzake vilimfanya awe na kiburi, akaanza kujiinua. Isaya 14:13-14. Tunajifunza kwamba, kiburi ni sumu mbaya sana katika maisha ya viumbe vya Mungu.

Kiumbe akiwa na kiburi husababisha mambo yafuatayo:

1. **Maanguko na Aibu:** Mithali 16: 18-20 Kiburi hutangulia uangamivu na aibu ya ghafla. Mtu mwenye majivuno huishia kudhalilika.
2. **Kujitenga na Mungu:** Kulingana na maandiko, mwenye kiburi ni chukizo kwa Bwana na hukosa neema na msaada wake.
3. **Migogoro na Ugomvi:** Kiburi huzaa ubishi, dharau, na mashindano ambayo huharibu amani na kuleta ugomvi kazini au kwenye jamii.
4. **Kuharibu Uhusiano na Familia:** Tabia ya kutokubali kukosolewa na kujiona bora huwavunja moyo na kuwatenga wale walio karibu nawe, hadi kuvunja ndoa au nyumba.
5. **Kukosa Ukuzi na Ushauri:** Mwenye kiburi ni mgumu kushaurika; hawezi kujifunza mapya wala kujirekebisha anapokosea. Pamoja na kushauriwa shetani hakuweza kukubali. Kiburi huondoa busara, hekima na maarifa.

Maandiko yanasema baada ya kuanzisha uasi, kukawa na vita mbinguni. Shetani alifanikiwa kushawishi malaika wengine kumfuata yeye. Kila wakati kunapotokea upinzani kwa wenye mamlaka au kwenye mfumo daima wapo siku zote wanaofuata mkumbo.

Maandiko yanabainisha kuwa wale wote waliomfuata yeye walitupwa pamoja naye. Huwezi kushindana na Mungu wakashinda. Mwanadamu hawezi kushindana na kanisa la Mungu analolichunga kama mboni ya Jicho lake akafanikiwa.

DHORUBA KWA WANADAMU

Baada ya shetani kushindwa na kutupwa chini aliendeleza roho yake ya uasi kwa viumbe vya Mungu. Wazazi wetu walipewa tahadhari juu ya dhoruba iliyokuwa imetokea mbinguni. Wakapewa maonyo na Mungu mwenyewe ambaye alikuwa akiwatembelea mara kwa mara katika bustani ya Edeni, wakapewa maonyo na malaika wa Bwana walikuwa wakitumwa mara kwa mara lakini basi hawakifanyia kazi sauti ya Bwana. Shetani alijivika vazi la nyoka na kisha akatoa udanganyifu wake kwa wazazi wetu na kwa bahati mbaya wakaufanyia kazi udanganyifu wake.

MATOKEO YA KUTOSIKIA SAUTI YA BWANA. (Mwanzo 3)

Wazazi wetu Adamu na mkewe waliishia kula tunda la mti wa ujuzi wa mema na mabaya baada ya kuwa wamekataa kutii sauti ya Bwana iliyokuwa ikisika kwao ikiwasihi watengane. Hivyo basi baada ya kuasi amri na kuvunja maagizo ya Mungu kulikuwa na matokeo yafuatayo:

- Wakapoteza utukufu waliokuwa nao, wakajiona wako uchi
- Mahusiano yako yao kijamii yakawa siyo mazuri-upendo kupungua, kulaumiana nk
- Uwezo wao wa kiakili ukaanza kupungua
- Mahusiano yao na Mungu Kiroho yakapungua-wakaanza kumwogopa Mungu Mwanzo 3:8- wakaanza kujificha uso wake.
- Hawakuweza kuonana au kuwasiliana tena uso kwa uso na Mungu
- Hali ya hewa ikabadilika, uchumi na maisha yote yakabadilika na kufuatiwa - kula kwa jasho na taabu.

TUMAINI LAANZISHWA EDENI

Maandiko matakatifu yanasema Bwana Mungu akawatembelea wanadamu hawa katika makazi yao. Sauti yenye matumanini ilisikika kwao ikiwatafuta. Mungu sio kwamba alikuwa hajui kilichokuwa kimefanyika, siyo kwamba hakujua mahali walipokuwa wamejificha. Mwangwi wa sauti yake ulikuwa na maana maalumu kwa wanandoa hawa.

UKO WAPI ADAM?

Swali hili kwa Adam halikumaanisha sehemu walipokuwa wamejificha (Geographical location). “Uko wapi Adam” Biblia imetumia neno “*Ayeka?*” (הָיָא) ikimaanisha maana kuu mbili

1. **Mwaliko wa Kujitafakari;** Mwenyezi Mungu alijua hasa mahali ambapo Adamu alikuwa amejificha kimwili. Kwa kumuuliza “Ayeka,” Mungu alikuwa akimwalika Adamu kutambua aliko kiroho na kihisia baada ya kufanya dhambi ya kwanza.
2. **Mwito wa Uwajibikaji:** Mungu alitumia ufunguzi huu mpole kumpa Adamu nafasi ya kutubu na kuchukua uwajibikaji bila kumkatia hukumu mara moja. Badala ya kumshutumu mara moja, Mungu alifungua nafasi ya mazungumzo. Kwa hiyo katika Bustani Edeni, dhambi ilipoingia, kitu cha kwanza kilichoharibika si mazingira, bali ni **nafasi ya mwanadamu mbele ya Muumba wake**. Swali “Uko wapi?” si swali la kijiografia; ni swali la mahusiano na uwajibikaji. Dhambi ni mbaya sana ilisababisha kujitenga na Kujificha kutoka kwa Mungu. Ilisababisha kupoteza ujasiri. Kabla ya dhambi, Adamu na Hawa walifurahia sauti ya Mungu ikitembea bustanini. Baada ya dhambi, sauti ileile ikawa chanzo cha hofu. Binadamu anapofanya makosa, hujaribu kujificha au kujitengenezea “mavazi” ya visingizio. Huwezi kujificha mbele za Mungu. Yale unayofikiri yanasitiri uchi wako, mbele za Mungu hayatoshi.
3. **Ni sauti ya Matumaini na urejeshwaji wa mahusiano mapya.** Yeye Ndiye Anayetutafuta sisi. Hataki tupotee katika uharibifu, anatumani sana tujitambue hali zetu, anahitaji tujitafakari na tufanye maamuzi ya kurudisha mahusiano yetu na yeye. Upendo kwa upendo wake mkuu alichukua hatua ya kurudisha mahusiano ambayo yalikuwa yamevunjwa na kukanyagwa chini. Mungu alianzisha jambo jipya kwa jamii ya wanadamu. Mpango wa Ukombozi ambao ulikuwa umetayarishwa kabla ya kuwekwa kwa Misingi ya ulimwengu ukawa umekuwa dhahiri kwa jamii ya wanadamu kama Jambo jipya la kumkomboa mwanadamu Mwanzo 3:15.

WITO: Mungu wetu ni Mungu wa mambo mapya. Ni Mungu muumbaji mwenye upendo ametupenda jinsi kama tulivyo. Anahitaji atufanye tuwe viumbe vipya ndani yake. Anahitaji kujitafakari na kufanya maamuzi sahihi. Mara nyingi tumekuwa tukitenda dhambi na kujificha lakini Mungu anatuona. Yawezekana hatujawa mawakili waaminifu kwa na tumejificha katika hali ngumu ya maisha/uchumi. Yawezekana tumekuwa kuwa hatufanyi kazi ya utume, tumekuwa watu wa kuja na kusali tu na kwenda nyumbani kuendelea na majukumu yetu ya kila siku kwa na kujifichwa kwenye visingizio vya kazi nyingi, kutafuta mkate wa kila siku, kusema mimi sina karama, au kusema watu ni wagumu, nk lakini Sauti ya Mungu inasema uko wapi?

Mungu anasema kuptia kanisa lake “SautiMoja27Utume kwa Wote” Je Uko tayari kufungamana katika Utume? Uko Tayari kutumia muda wako kusoma Maneno ya Unabii (Biblia na vingine vitabu vya roho ya Unabii? na Je utakuwa tayari kujielekeza katika kutimiza agizo la utume tuliloagizwa na Kristo? Mungu atusaidie tuisikie sauti yake ili tuwe na sauti moja na nia moja tu iliyokuwamo ndani ya Kristo Yesu.

MAMBO YA KUOMBEA: Tuombee usomaji wa neno la MUNGU. Neno la Mungu ni taa ya miguu yetu na mwanga wa njia zetu katika maisha ya kila siku. Tunahitaji kuomba ili waumini wapate hamu ya kulisoma, kulitafakari, na kupata ufunuo wa Roho Mtakatifu kupitia Maandiko Matakatifu.

Mhudumu / Kanisa laweza kuongeza mambo mengine ya kuombea katika nafasi hii.

Somo La Tatu

KARAMA YA UNABII KATIKA AGANO LA KALE

Na Pr Keshi Martin Malehiwa

Mkurugenzi wa huduma za Uchapishaji na Roho ya Unabii

Conferensi ya Kusini Mashariki (SEC)

Fungu la leo: **Amosi 3:7** inasema: *“Hakika Bwana MUNGU hatafanya neno lo lote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake.”*

A: Utangulizi: Unabii katika Agano la Kale ni ujumbe ambao Mungu aliwapa watu aliowaita ili waufikishe kwa wengine. Mara nyingi tunaposikia neno unabii, tunafikiria juu ya utabiri wa mambo yajayo. Hilo ni sehemu ya unabii, lakini si kazi yake yote. Manabii waliwaita watu watubu, walikemea dhambi na udhalimu, waliwafariji waliokuwa katika mateso, na waliwasaidia watu kuelewa mapenzi ya Mungu.

Kwa msingi wa Biblia, unabii katika Agano la Kale unaonyesha mpango wa Mungu wa wokovu katika historia. Unaanza na ahadi ya Mungu baada ya mwanadamu kuanguka dhambini katika Mwanzo 3:15, na unaendelea kuelekeza macho yetu kwenye ushindi wa Mungu na ufalme wake wa milele.

B: NENO “NABII” LILIPOTUMIKA KWA MARA YA KWANZA KATIKA AGANO LA KALE

Tunapaswa kutofautisha kati ya ahadi ya kwanza yenye maana ya kinabii na mtu wa kwanza kuitwa nabii. Katika Mwanzo 3:15, baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi, Mungu alitangaza uadui kati ya nyoka na uzao wa mwanamke. Wakristo wanaona ndani ya ahadi hiyo mwanzo wa habari njema kwamba uovu hautashinda milele. Tunapoisoma katika mwanga wa Maandiko mengine, tunaona ushindi huo ukitimia katika Kristo.

Mtu wa kwanza kuitwa **“nabii” waziwazi** katika mpangilio wa Agano la Kale ni **Ibrahimu**. Katika **Mwanzo 20:7**, Mungu alimwambia Abimeleki kuhusu Ibrahimu: **“maana huyo ni nabii, naye atakuombea.”** Jambo hili linatufundisha kwamba huduma ya nabii haikuhusu kutangaza ujumbe tu. Ibrahimu pia aliitwa **kuwaombea wengine**.

C: NABII NI NANI KATIKA AGANO LA KALE?

Nabii ni mtu **aliyeitwa na Mungu kupokea na kufikisha ujumbe wake kwa uaminifu**.

Neno la Kiebrania linalotafsiriwa “nabii” ni navi’. Biblia pia hutumia majina kama mwonaji katika 1 Samweli 9:9, mtu wa Mungu katika 1 Samweli 9:6, mjumbe wa Bwana katika Hagai 1:13, na mlinzi katika Ezekieli 3:17. Majina hayo yanaonyesha kwamba nabii alipokea ujumbe, aliutangaza, na alikuwa na wajibu wa kuwaonya watu.

Mungu alipomwambia Musa kwamba Haruni atakuwa nabii wake katika **Kutoka 7:1**, alimpa mfano unaosaidia kuelewa kazi hiyo. Nabii ni yule anayesema kwa niaba ya Mwingine. Haruni angesema ujumbe aliopewa na Musa. **Vivyo hivyo, nabii wa Mungu hakutakiwa kutangaza mawazo yake mwenyewe kana kwamba ni neno la Mungu; alipaswa kuwa mwaminifu kwa ujumbe aliokabidhiwa.**

Nabii si mtabiri wa mambo yajayo pekee. Musa aliongoza na kufundisha. Nathani alimkabili mfalme Daudi kuhusu dhambi yake katika 2 Samweli 12:1–13. Eliya aliwaita Waisraeli waache ibada ya Baali katika 1 Wafalme 18:21. Isaya alionya kuhusu dhambi na kutangaza tumaini la wokovu. Yeriahi aliionya Yuda kuhusu hukumu, lakini pia alitangaza ahadi ya agano jipya katika Yeriahi 31:31–34.

Huduma ya kinabii haikuwa ya wanaume pekee. **Miriamu** anaitwa nabii wa kike katika Kutoka 15:20. **Debora** alikuwa nabii wa kike na mwamuzi katika Waamuzi 4:4. **Hulda** alipeleka ujumbe wa Mungu kwa wajumbe wa mfalme Yosia katika 2 Wafalme 22:14–20.

Ellen G. White anaeleza katika *Education*, ukurasa wa 46, kwamba kwa maana ya juu zaidi, nabii alikuwa mtu aliyenena kwa uvuvio wa moja kwa moja na kuwafikishia watu ujumbe alioupokea kutoka kwa Mungu. Maelezo yake yanasisitiza kwamba mamlaka ya nabii wa kweli yanatokana na **Mungu aliyetoa ujumbe**, si umaarufu au cheo cha nabii mwenyewe.

D: Mungu Aliwasilianaje na Watu katika Agano la Kale?

Mungu alitumia njia mbalimbali kuwasiliana na watu. Wakati mwingine **alisema moja kwa moja**. Alisema na Adamu na Hawa baada ya dhambi katika Mwanzo 3:8–19, alimwita Ibrahimu katika Mwanzo 12:1–3, na alimwita Musa katika kichaka kilichokuwa kinawaka moto katika Kutoka 3:4–10. Hesabu 12:7–8 inaonyesha kwamba mawasiliano ya Mungu na Musa yalikuwa ya kipekee; hatupaswi kudhani kwamba kila nabii alipokea ujumbe kwa namna ileile.

Mungu pia alitumia **maono na ndoto**. Katika Hesabu 12:6 alisema kwamba akiwapo nabii, atajifunua kwake katika maono na kusema naye katika ndoto.

Danieli alipokea maono kuhusu falme na mambo ambayo yangetokea baadaye, kama tunavyoona katika Danieli 7. Yusufu aliota ndoto zilizohusu maisha ya familia yake katika Mwanzo 37:5–11.

Wakati mwingine Mungu alitumia **malaika kueleza ujumbe**. Kwa mfano, katika Danieli 8:15–19 na 9:21–23, malaika alimsaidia Danieli kuelewa mambo aliyokuwa ameonyeshwa. Malaika alikuwa mjumbe na mfasiri wa ujumbe; chanzo cha ujumbe kilikuwa Mungu.

Mungu pia aliwasiliana kupitia **maagizo yake yaliyoandikwa na kusomwa hadharani**. Kumbukumbu la Torati 31:9–13 inaonyesha umuhimu wa kuisoma sheria mbele ya watu. Manabii wa baadaye waliwakumbusha watu yale ambayo Mungu alikuwa amekwisha kuwaagiza. Hivyo, unabii wa kweli haukuwapa watu sababu ya kupuuza Neno la Mungu walilokuwa nalo tayari.

Katika hali nyingine, ujumbe uliwasilishwa kwa **vitendo vyenye ishara**. Yeremia alivaa nira ili kufanya ujumbe kuhusu Babeli uonekane wazi katika Yeremia 27:1–11. Ezekieli alifanya vitendo vya ishara kuhusu hukumu iliyokuwa inaikaribia Yerusalemu katika Ezekieli 4–5. Mungu alitumia vitendo hivyo ili watu waone kwa macho uzito wa ujumbe.

Ingawa njia za kupokea ujumbe zilitofautiana, chanzo cha unabii wa kweli kilikuwa kilekile. **2Petro 1:21** inasema kwamba wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu. Nabii alikuwa mwanadamu mwenye lugha, tabia na mazingira yake, lakini ujumbe aliokabidhiwa ulitoka kwa Mungu.

JUKUMU LA MANABII KATIKA AGANO LA KALE

Kwanza, manabii **waliwaita watu wamrudie Mungu**. Walikemea hali ya kuendelea na ibada kwa nje huku mioyo na matendo ya watu vikiwa mbali na Mungu. Eliya aliwauliza Waisraeli katika 1 Wafalme 18:21: **“Mtasita-sita katikati ya mawazo mawili hata lini?”** Lengo la swali hilo lilikuwa kuwaita wafanye uamuzi wa kumwabudu Bwana kwa uaminifu.

Pili, manabii **walitetea haki na rehema**. Amosi aliwakemea waliowakandamiza maskini huku wakiendelea na taratibu za kidini, kama tunavyoona katika Amosi 5:11–24. Mika 6:8 inasema kwamba Mungu anamtaka mwanadamu **“kutenda haki, na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako.”** Kwa manabii, uaminifu kwa Mungu ulipaswa kuonekana katika namna watu walivyowatendea wengine.

Tatu, manabii **walitoa onyo kabla ya hukumu**. Yeremia alionya Yuda kuhusu matokeo ya kuendelea kuasi, hasa katika Yeremia 25:8–11. Onyo la

Mungu lilikuwa nafasi ya watu kusikiliza na kutubu. Hata hivyo, 2 Mambo ya Nyakati 36:15–16 inaeleza kwamba watu mara nyingi waliwadharau wajumbe wa Mungu.

Nne, manabii **walitoa tumaini wakati wa mateso**. Isaya aliwafariji watu wa Mungu kwa ujumbe kwamba hawakuwa wamesahauliwa katika Isaya 40:1–5. Yeremia alitangaza kwamba Mungu angefanya agano jipya na kuandika sheria yake miyoyoni mwa watu katika Yeremia 31:31–34. Ezekieli aliona maono ya mifupa mikavu katika Ezekieli 37:1–14, akionyesha uwezo wa Mungu wa kurejesha uhai na tumaini mahali ambapo watu waliona mwisho tu.

Tano, manabii **walielekeza kwa Masihi na ufalme wa Mungu**. Isaya alizungumzia mtawala anayehusishwa na amani katika Isaya 9:6–7 na mtumishi anayechukua mateso ya wengine katika Isaya 53:4–6. Mika 5:2 inahusisha Bethlehemu na mtawala atakayetoka Israeli. Katika Danieli 7:13–14, mmoja aliye “mfano wa mwanadamu” anapokea ufalme usiopita. Wakristo husoma mafungu hayo katika mwanga wa Yesu Kristo, huku wakizingatia pia mazingira ya kila unabii.

Sita, manabii **walionyesha kwamba Mungu anatawala historia**. Maono ya Danieli 2 na 7 yanaonyesha falme za dunia zikiinuka na kuanguka, lakini ufalme wa Mungu ukidumu milele. Kwa Waadventista wa Sabato, Danieli 8:14 ni sehemu muhimu ya kujifunza huduma ya Kristo katika patakatifu pa mbinguni na hukumu inayotangulia kurudi kwake.

Mwisho, manabii waliwasaidia watu **kupima madai ya kiroho**. Kumbukumbu la Torati 13:1–4 inaonya kwamba hata ishara ya kushangaza haifanyi ujumbe unaowapeleka watu mbali na Mungu kuwa wa kweli. Kumbukumbu la Torati 18:20–22 inaonya kuhusu kusema kwa uongo kwa jina la Mungu. Isaya 8:20 inawaelekeza watu kupima ujumbe kwa ufunuo ambao Mungu ametoa. Kwa hiyo, kumheshimu nabii wa kweli hakumaanishi kuacha kuchunguza ujumbe wake kwa Maandiko.

Mifano ya Manabii na Unabii Wao katika Agano la Kale

Ibrahimu aliitwa nabii katika Mwanzo 20:7. Alipokea ahadi kwamba kupitia uzao wake mataifa ya dunia yangebarikiwa, kama ilivyo katika Mwanzo 12:1–3. Pia alikuwa mwombezi. Maisha yake yanaonyesha kwamba Mungu alimwita mtu mmoja akiwa na kusudi pana la kuyabariki mataifa.

Musa alitumwa kutangaza ukombozi wa Israeli kutoka Misri katika Kutoka 3:7–10. Aliwafundisha watu maagizo ya Mungu na kuwaonya kuhusu

matokeo ya uaminifu au kutotii katika Kumbukumbu la Torati 28–30. Huduma yake inaonyesha kwamba ukombozi wa Mungu uliwaita watu kuishi katika uhusiano wa agano naye.

Samweli alipeleka ujumbe wa Mungu katika kipindi ambacho Israeli ilianza kuwa na wafalme. Alimkemea Sauli na kumkumbusha kwamba kumtii Mungu ni jambo la msingi kuliko kutoa dhabihu bila utii, kama inavyoonekana katika 1 Samweli 15:22–23. Mfano wake unaonyesha kwamba hata mfalme alipaswa kusikiliza Neno la Mungu.

Nathani alimfikishia Daudi ahadi kuhusu nyumba yake katika 2 Samweli 7:12–16. Baadaye alimkabili Daudi kuhusu dhambi yake katika 2 Samweli 12:1–13. Nathani anatukumbusha kwamba nabii wa kweli hakupaswa kuficha ukweli kwa sababu ya woga wa mwenye mamlaka.

Eliya alikabili ibada ya Baali na kuita taifa limtambue Bwana katika 1 Wafalme 18:17–39. Ujumbe wake haukuwa wa majadiliano ya kidini pekee; uliwataka watu waache kujigawa kati ya ibada ya Mungu na ibada ya sanamu.

Isaya aliona utakatifu wa Mungu na kuitikia wito wake katika Isaya 6:1–8. Aliwakemea watu kuhusu dhambi, lakini pia alitangaza ahadi za tumaini katika Isaya 9:6–7 na ujumbe wa mtumishi mwenye mateso katika Isaya 53:4–6. Kitabu chake kinaonyesha hukumu ya Mungu na neema yake kwa pamoja.

Yeremia aliionya Yuda kuhusu uvamizi na uhamisho katika Yeremia 25:8–11. Aliwapa watu pia tumaini la kurejea kutoka uhamishoni katika Yeremia 29:10–14 na akatangaza agano jipya katika Yeremia 31:31–34. Ujumbe wake unatufundisha kwamba kusema ukweli kuhusu hukumu hakuzuii kutangaza tumaini la Mungu.

Danieli alitafsiri ndoto ya Nebukadneza katika Danieli 2:27–45 na alipokea maono kuhusu falme, hukumu na ufalme wa Mungu katika Danieli 7–8. Mafunzo yake yanaonyesha kwamba mamlaka za dunia ni za muda, lakini ufalme wa Mungu ni wa milele.

Mika alikemea viongozi waliopotosha haki katika Mika 3:9–12, akatangaza ahadi kuhusu mtawala atakayehusishwa na Bethlehemu katika Mika 5:2, na akafundisha maisha ya haki, rehema na unyenyekevu katika Mika 6:8. Kwa Mika, kutarajia kazi ya Mungu ya baadaye hakukuondoa wajibu wa kutenda haki leo.

Hulda alipokea na kutoa ujumbe wa Mungu wakati wajumbe wa mfalme Yosia walipokuja kumuuliza katika 2 Wafalme 22:14–20. Huduma yake

inatukumbusha kwamba Mungu aliwaita pia wanawake kuwa wajumbe wake, na kwamba ujumbe wao ulipaswa kusikilizwa kwa uzito.

Mifano hii inaonyesha kwamba unabii wa Agano la Kale haukuwa wa aina moja. Ujumbe mwingine ulihusu tatizo la wakati ule; mwingine uliwahimiza watu waitikie ili kuepuka hukumu; na mwingine ulielekeza mbele kwa Masihi na ufalme wa Mungu. Ndiyo maana ni muhimu kusoma **sura nzima na mazingira ya kihistoria** kabla ya kutoa maana au matumizi ya unabii fulani.

Hitimisho: Unabii wa Agano la Kale unamfunua Mungu ambaye **huwaonya watu kabla ya hukumu, huwaita watubu, na huwapa tumaini hata wanapokuwa katika shida.** Ibrahimu aliombea wengine; Musa aliongoza; Eliya alikabili uasi; Isaya alitangaza tumaini; Yeremia alionya; na Danieli alionyesha kwamba historia ya dunia haiko nje ya mamlaka ya Mungu.

Kwa hiyo, kujifunza unabii kunapaswa kutuongoza zaidi ya hamu ya kujua matukio yajayo. Kunapaswa kutufanya **tusikilize Neno la Mungu, tutende haki, tutubu dhambi, na kumtumaini Yesu Kristo.** Danieli 7:14 inatuelekeza kwenye ufalme ambao **“hautapita kamwe.”** Hilo ndilo tumaini kuu linalobaki wakati falme na nguvu za dunia zinapita.

Tuna mengi ya kujifunza kutoka katika huduma na jumbe za manabii mbalimbali wa Agano la Kale. Vivyo hivyo, leo hii tunajifunza namna ya kupokea na kuyatumia maono, mafundisho, maelekezo, na maonyo tunayoyapata kupitia Maandishi ya Mjumbe wa Bwana, Ellen G. White yaliyo na manufaa kwa wokovu wetu na huduma yetu kwa ulimwengu. Bwana aliyenena zamani kupitia kwa manabii wake bado ananena nasi leo. Je, unayo nafasi ya kuisikia sauti ya Mungu ikizungumza nawe kupitia machapisho haya? Umeyashiriki vipi maonyo na mafundisho haya na familia yako pamoja na majirani zako?

Swali la kutafakari: Ikiwa manabii waliwaita watu wa nyakati zao watubu, watende haki na kumwabudu Mungu kwa uaminifu, ni sehemu gani ya wito huo tunayohitaji kuisikia zaidi leo?

MAMBO YA KUOMBEA: Tuombee waumini wote tuamke na kuihubiri injili. Wito wa kutangaza habari njema unahitaji msisimko na jitihada za kila muumini bila kusita. Tunapaswa kuomba ili Mungu atupe ujasiri na nguvu za kutoka na kuwafikia watu wote wenye kiu ya neno lake.

Mhudumu / Kanisa laweza kuongeza mambo mengine ya kuombee katika nafasi hii.

Somo La Nne

KARAMA YA UNABII KATIKA AGANO JIPYA

Na Mchungaji Joseph Jackson Chengula.

Meneja wa shirika la usambazaji wa machapisho (HHES)

Unioni ya kusini mwa tanzania (STUM).

Utangulizi: Karama ya unabii ni nini? Ni zawadi ya Roho Mtakatifu anayopewa mtu na MUNGU kwa kuona maono na ndoto ili kuweza kusikia sauti ya MUNGU nakuyasema kwa watu kama ujumbe sasa uliotoka kwa MUNGU mwenyewe.

1Korintho 14:3 *Bali anayehutubu husema na watu maneno ya kuwajenga, na kuwafariji, na kuwatia moyo*”

Hapa kuna kazi tatu za Karama ya Unabii:

1. **Kujenga** Kumjenga mtu kiroho, Kumuimarisha Imani yake.
2. **Kumfariji**, Kumpa mtu faraja, Tumaini wakati wa changamoto na katika hali ya kupitia mambo magumu.
3. **Kumtia moyo**, kumtia moyo ili mtu asiache kumtumaini MUNGU katika maisha yake.

MUHIMU: Mwenye karama ya unabii: Ni mtu yeyote aliyejazwa Roho mtakatifu, anaweza kutabiri kwa wakati Fulani ulioamriwa. (Habakuki2:2,4.)

Nabii ni cheo au wito maalumu wa maisha, nabii anaishi maisha ya nabii kila siku. Karama ya Unabii ni karama kutoka kwa Roho Mtakatifu ya kusema fikra (au nia) za Mungu kwa watu ili kuwajenga, kuwatia moyo, na kuwafariji.

Je, Bwana Mungu anaweza kumchagua mtu yo yote ili aweze kuwa nabii wake? Biblia inasemaje? Yoeli 2:28_30. “Hata itakuwa, baada ya hayo, kwamba nitamimina roho yangu juu ya wote wenye mwili, nawana wenu, wa kiume na wa kike, watatabiri, Wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono. Tena juu ya watumishi wenu wanaume na wanawake, katika siku zile, nitamimina roho yangu. Nami nitaonesha mambo ya ajabu katika dunia, damu, na moto na minara ya moshi”

Bwana Mungu alijipatia manabii katika Historia ya maandiko matakatifu, katika Agano la kale na hata katika Agano jipya, wakike na hata wa kiumbe.

Baadhi ya Manabii;

- 1. Bwana YESU Kristo.** Pia aliitwa nabii mkuu katika siku zile soma Mathayo 21:11. Lakini pia, hebu tuone fungu hili, Luka 24:19, “Akawauliza, mambo gani? Wakamwambia, mambo ya Yesu wa Nazareti, aliye kuwa mtu nabii mwenye uwezo katika kutenda na kunena mbele za MUNGU na watu wote. Soma tena Yohana 6:14, “Basi watu wake walipoiona ishara aliyoifanya, walisema, hakika huyu ni nabii yule ajaye ulimenguni.”
- 2. Yohana mbatizaji_ (John the Baptist).** Huyu ni nabii wa kwanza wa Agano Jipya. Yohana alihubiri kuhusu ujio wa Yesu baadae. Yohana sauti ya mtu aliye nyikani, soma Mathayo 11:9_11 Hajatokea mtu katika wazao wa wanawake aliye mkuu kuliko Yohana mbatizaji, Lakini aliye mdogo katika ufalme wa Mbinguni ni mkuu kuliko yeye.
- 3. Agabo (Agabus)_** Huyu ni nabii ambaye alitabiri kuhusu njaa kubwa na kufungwa kwa Paulo. “Basi tulipokuwa tukikaa huko siku nyingi, nabii mmoja jina lake Agabo akashuka kutoka Uyahudi 11 Alipotufikia akautwaa mshipi wa Paulo, akajifunga miguu na mikono akasema, Roho Mtakatifu asema hivi, hivyo ndivyo wayahudi wa Yerusalemu watakavyo mfunga mtu mwenye mshipi huu, nao watmtia katika mikono ya watu wa mataifa” Mdo 21:10,11. “Siku zizo hizo Manabii waliteremka kutoka Yerusalemu hadi Antiokia na tulipo kusanyika akasimama mmoja wao, jina lake Agabo, akaonesha kwa uweza wa Roho Mtakatifu kwamba njaa kubwa duniani itakuja karibu katika dunia nzima, nayo nayo ikatukia katika siku za Klaudio” (Mdo 11:27,28).
- 4. Binti 4 Wa Filipo Mwinjilisti_** Hawa nao walikuwa na karama ya unabii na MUNGU aliwatumia sana. “Mtu huyu alikuwa na binti wane, Mabikira waliokuwa wakitabiri” (Mdo 21:9). Hata mabinti wanapewa karama ya unabii usijishushe MUNGU, atakutumia kwa wakati wake.
- 5. Yohana (John)_** Mwandishi wa kitabu cha Ufunuo, Ni nabii wa nyakati za mwisho. “Heri asomaye na wao wayaskiao maneno ya unabii huu na kuyashika yaliyoandikwa humo kwa maana wakati uko karibu” (Ufunuo 1:3). “Na tazama, naja upesi, heri yeye ayashikaye maneno ya unabii wa kitabu hiki” (Ufunuo 22:7)
- 6. Manabii ndani ya kanisa_** Basi huko Antiokia, katika kanisa lililokuwako, palikuwa na manabii na walimu, Barnaba, na S i m e o n i aitwaye Niger, na Lukio, na Manaeni, na Sauli” (Mdo 13:1). “Naye alitoa wengine kuwa Mitume, na wengine kuwa Manabii na wengine kuwa Wainjilisti” (Efeso 4:11).

Sifa za nabii wa kweli.

Biblia inatufunulia sifa za Nabii wa kweli kama ifuatavyo:

1. Unabii anaoutoa lazima ukubaliane na Maandiko ya Biblia. (Isaya 8:20)
2. Unabii anaoutoa lazima uweze kutimia. (Kumbukumbu 18:21, 22).
3. Nabii wa kweli atambue kufanyika mwili kwa Bwana Yesu Kristo. (1 Yohana 4:2,3)
4. Nabii wa kweli anapaswa adhihirishe mafundisho yake katika maisha yake. Mtawatambua kwa matendo yao. (Mathayo 7:16,18-20).

Ni muhimu kufahamu kwamba maisha na mafundisho ya Mama Ellen G. White yanakidhi kikamilifu sifa za kuwa Nabii wa kweli katika nyakati hizi za siku za mwisho. Ni fursa kubwa na ya pekee iliyoje kwa washiriki wa kanisa kusoma na kufuatilia mafundisho ya Nabii huyu wa Mungu na kujiandaa kwa ajili ya kuja kwa Bwana Yesu Kristo mara ya pili?

Tafakari juu ya machapisho yanayotokana na kipawa cha Nabii huyu wa Mungu, “Machapisho ambayo aliandika ni zaidi ya vitabu 80, vijizuu 200 na magazeti, 4,600. Mahubiri, shuhuda, na barua huunda zaidi ya kurasa 60,000 kwa mkono wake.” (Seventh-day Adventist Believe, A Biblical Expository of Fundamental Doctrines, 1988, Ukurasa, 226). Unaweza kuwa na hisia kwamba kwa uandishi huo na kweli alizozandika, unaweza kuwa na hisia kwa kweli kwamba, alipokuwa anaandika alikuwa ana ongozwa na Roho Mtakatifu.

Tunapaswa kuvisoma vitabu hivi kwa bidii maana ndio urithi wetu kupitia kwa huduma ya huyu mtumishi wa Mungu, Ellen G. White. Ambaye akafanya kazi ya unabii kwa muda wa miaka 70 jumla ya miaka yake aliyoishi duniani ni miaka 87 na julai 16, 1915 alilala usingizi wa mauti. MUNGU alijifunua kwake kwa miaka hiyo kwa njozi mbalimbali na maono kwa kiwango cha juu sana.

Maono hayo yameandikwa katika vitabu mbali mbali kwa ajili yetu tunapoelekea mwisho wa ulimwengu.

MUHIMU: Uwepo wa mafunuo haya ya Bwana Mungu kupitia kwa uandishi wa Mjumbe wa Mungu, Ellen G. White, ni urithi wa maana sana katika kanisa la Bwana Mungu wetu na ulimwengu mzima kwa ujumla. Uwepo wa machapisho haya ya Bwana Mungu ambayo hayapitwi na wakati hutuwajibisha mara mbili, kwanza kwamba tuwe wasomaji na watendaji waaminifu wa vitabu na machapisho wa Nabii huyu.

Jambo la pili, tunatakiwa kushiri kweli zinazopatikana katika vitabu na

machapisho haya na watu wengine katika ulimwenu huu kabla ya kuja kwa Kristo.

Kupitia kwa mafundisho yake adhimu sana, leo tunakumbushwa hitaji letu kuu katika miisho hii ya dunia. **Hitaji Muhimu**, “Hitaji kubwa la kanisa la Masalio siyo ongezeko la washiriki, Wahubiri Zaidi, au vifaa Zaidi sasa hitaji kubwa leo ni watu waume na wake waliojazwa na Roho Mtakatifu. Tuna nyumba kubwa ya kufanyia kazi mbali mbali, tuna vitabu vingi ulimwenguni Tuna shirika kubwa Zaidi ulimwenguni. Lakini kumaliza kazi ya MUNGU, Yatupasa tupokee kwa upya kila siku ubatizo wa Roho Mtakatifu. Nani atajibu, bila kuficha lolote moyoni, wito huu mkuu wa Saa hii ya Kufikia mwisho wa historia ya dunia?” Kutayarisha Njia, (Sehemu ya pili) Ellen G. White, TAP, 1991 uk.87.

Jambo la pekee ni kwamba, kipawa hiki cha pekee kinajidhihirisha katika nyakati za mwisho kama moja ya alama za utambulisho wa kanisa la kweli kama ilivyoandikwa katika kitabu cha Ufunuo 12:17, “Joka akamkasirikia yule mwanamke akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia hao wazishikao amri za MUNGU na kuwa na ushuhuda wa Yesu, naye akasimama juu ya mchanga wa bahari.”

Maswali ya kutafakari na kujadili kwa kina

1. Tutachukua hatua gani kama kanisa ili kuamsha na kuimarisha ari ya usomaji wa Biblia na vitabu vya Roho ya Unabii miongoni mwa waumini?
2. Tutawasaidiaje kwa upendo na hoja za Kimaandiko wale wanaotilia shaka Ujumbe na Kanisa la Mungu la Waliosalia?
3. Ni mbinu gani za kichungaji na za kiroho tutakazozitumia ili kuwafikia na kuwarudisha kondoo wa Mungu waliopotea, ambao wao wenyewe wanajiona hawajapotea?
4. Ni mbinu gani madhubuti tutakazozitumia ili kufikisha machapisho ya Roho ya Unabii kwa watu wote ulimwenguni?
5. Ni mambo gani ya msingi yanayopaswa kuboreshwa katika Idara ya Roho ya Unabii ili kuongeza ufanisi wa huduma hii?

Mbaraka wa Hitimisho: Mungu akubariki sana unaposhiriki kikamilifu katika usambazaji wa vitabu vya kutosha juma hili. Shiriki baraka hizi kwa kugawa vitabu kwa watu wengi zaidi wiki hii!

MAMBO YA KUOMBEA: Tuwaombe watu waliorudi nyuma, MUNGU awarudishe kwenye kanisa lake. Wengi wamekumbana na changamoto au majaribu yaliyowafanya wajitenge na ushirika wa kiroho. Ni wajibu wetu kuwaombea kwa upendo ili Mungu awape neema ya kutubu na kurejea nyumbani kwa furaha.

Mhudumu / Kanisa laweza kuongeza mambo mengine ya kuombea katika nafasi hii.

Somo La Tano

KARAMA YA ROHO YA UNABII KATIKA SIKU ZA MWISHO

Limeandaliwa na Mch Harold William Lissi

Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Uchapishaji na Roho ya Unabii –
Konferensi ya Nyanda za Juu Kusini

Fungu kuu: **Ufunuo 12:17; 19:10**, *“Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu; naye akasimama juu ya mchanga wa bahari.*

Nami nikaanguka mbele ya miguu yake, ili nimsujudie; akaniambia, Angalia, usifanye hivi; mimi ni mjoli wako na wa ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu. Msujudie Mungu. Kwa maana ushuhuda wa Yesu ndio roho ya unabii”.

Roho ya unabii ni mojawapo ya karama za Roho mtakatifu, ambapo Mungu mwenyewe alijifunua kwa baadhi ya watu aliowachagua na kuwapa ujumbe wake kwa njia ya maono, ndoto au njozi. Kupitia karama ya roho ya unabii, Mungu amelipa Kanisa lake ujumbe wenye kusudi la kulifundisha, kulionya, kulisahihisha, kuliongoza, kulijenga na kulitia moyo, ili waumini waweze kukua katika imani na kutembea katika mapenzi yake.

Uwepo wa karama ya roho ya unabii katika Kanisa la Mungu linaloishi katika siku za mwisho umeleta baraka kubwa na kudhihirisha kwamba Mungu analiongoza Kanisa lake katika nyakati zote kupitia karama ya unabii.

Mjumbe wa Mungu Ellen G. White anasema; *“Mungu ameahidi kutoa maono katika siku za mwisho; si kwa ajili ya kuwa kanuni mpya ya imani, bali kwa ajili ya kuwafaraji watu wake, na kuwarekebisha wale wanaopotoka kutoka katika kweli ya Biblia.”* *Early Writings*, p. 78.

Sifa mbili muhimu za kulitambua kanisa la Mungu (Ufunuo 12:17), ni **kuzishika amri za Mungu na kuwa na ushuhuda wa Yesu**. Tayari biblia imejifafanua yenyewe kuwa; **“ushuhuda wa Yesu” ni “Roho ya Unabii”** (Ufunuo 19:10). **Jinsi Mungu alivyoidhihirisha karama ya roho ya unabii katika kanisa lake.** Karama ya unabii ilidhihiliwa katika maisha na huduma ya Ellen G White ambaye alizaliwa mwaka 1827 na kufariki dunia mwaka 1915 (*Life Sketches of Ellen G. White*, chapter 1).

Karama hii ilianza kudhihirika katika maisha yake kupitia maono na njozi alizopokea baada ya kipindi kinachojulikana kama **“Kukatishwa Tamaa Kubwa” (The Great Disappointment)**, kilichotokea mwaka 1844. Kipindi hicho kilifuata baada ya William Miller kuhubiri na kutangaza kwamba Yesu angerrudi duniani mwaka huo.

Mjumbe wa Mungu, **Ellen G. White**, alipewa ujumbe wa kuwatia moyo waumini waliokuwa wamekata tamaa, ili kuwaimarisha na kuwahimiza waendele kumtumaini na kumngojea Yesu. Tangu alipopokea njozi yake ya kwanza mwishoni mwa mwaka 1844, Ellen G White aliendelea kutumiwa na Mungu kwa kupokea maono na njozi takatifu kwa takribani miaka 70 ya huduma yake. Jumbe alizopokea zilihusisha mafundisho, maonyo, masahihisho, maelekezo, kutia moyo, kwa lengo la kuwasaidia waumini kudumu katika imani na kuendelea kuwa waaminifu katika maisha yao ya Kikristo.

Swali ambalo unaweza kujiuliza kuhusu karama ya roho ya unabii ni hili; Katika dunia hii ambayo ina manabii wengi wa uongo, nawezaje kutambua kuwa mtu fulani ana karama ya kweli ya roho ya unabii?

Ni kweli neno la Mungu limetutahadharisha kuwa katika siku za mwisho watatokea manabii wengi wa uongo. Watafanya ishara na maajabu na kuwavuta watu wengi wawaamini na kudanganya wengi. Tusiamini kila roho, bali tuwapime wale wanaojisema kuwa wamepewa unabii kupitia kwa neno la Mungu. “Wapenzi, msiamini kila roho, bali ziharibuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani (1Yohana 4:1)”

Vipimo vya kutambua nabii wa kweli

1. Ujumbe wake Ukubariane na neno la Mungu. Isaya 8:20: *“Na waende kwa sheria na ushubuda; ikiwa hawasemi sawasawa na neno bili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi.”* Neno la Mungu, yaani Biblia, ndicho kiwango cha juu kabisa na kipimo cha madai ya mtu yeyote anayesema kuwa ana uvuvio au ameonyeshwa na Mungu kwa jambo lolote. Manabii lazima wapime na kulinganisha kile wanachosema na kile ambacho Neno la Mungu, yaani Biblia, linasema. Nabii wa kweli kamwe hatapingana na ukweli ambao tayari umefunuliwa katika Biblia, wala na ujumbe ambao Mungu aliwafunulia manabii waliotangulia na ambao umeandikwa katika Biblia. Mtume Paulo anatumieza kwamba, *“roho za manabii huwatii manabii”* (1 Wakorintho 14:32).

2. Amkiri Yesu kuwa ni Mwana wa Mungu na kwamba alikuja katika mwili 1 **Yohana 4:2**: *“Katika hili mwamjua Robo wa Mungu; kila robo ikiriyo kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatokana na Mungu.”* Kipimo hiki kinaweza kutumika kwa haraka kuwachunguza watu wanaodai kuwa manabii, lakini wanatoka katika dini zilizo nje ya Ukristo na hawamwamini Yesu kuwa ni Mwana wa Mungu, wala kwamba alikuja katika mwili. Hata hivyo, pamoja na kipimo hiki, si kila mtu anayelitaja jina la Yesu na kukiri kwamba Yesu ni Bwana tunapaswa kumwamini kuwa ni nabii wa kweli. Biblia inatuambia kwamba hata mashetani wanamkiri Yesu, wanaamini na kutetemeka (**Yakobo 2:19**). Kwa hiyo, kumkiri Yesu ni kipimo cha haraka, lakini si kigezo pekee cha kumtambua nabii wa kweli. Jambo lingine muhimu ni **kufanya mapenzi ya Mungu**.
3. Unabii anaoutoa utimie. **Yeremia 28:9**: *“Nabii atabiriye habari za amani, neno la nabii yule litakapotokea, ndipo nabii yule atakapojulikana, kuwa Bwana amemtuma kweli kweli.”* Kutimia kwa unabii uliotolewa ni kipimo kingine muhimu cha kutambua ikiwa mtu anaweza kuwa nabii wa kweli. Hata hivyo, kipimo hiki wakati mwingine kinaweza kuwa na changamoto katika kukitumia au kutambua matokeo yake, kwa sababu baadhi ya unabii huwa na masharti. Kwa mfano, Yona alitabiri kwamba baada ya siku arobaini Ninawi ingeamizwa. Hata hivyo, kulikuwa na sharti lililohusiana na mwitikio wa watu wa Ninawi. Kama wangetubu, Bwana asingewaangamiza Ninawi, kama ilivyotokea. Kwa hiyo, unabii wenye masharti hutegemea jinsi watu watakavyoitikia ujumbe uliotolewa.
4. Matunda yake au mwenendo wa maisha yake. Pamoja na kwamba hakuna mwanadamu mkamilifu, na kwamba manabii walikuwa wanadamu wenye dhambi na mapungufu mengine, nabii wa kweli atatambulikana kwa matunda yake. Nabii wa kweli atakuwa amejitoa kikamilifu kufuata kanuni za Neno la Mungu na ataishi katika mwenendo mzuri wa maisha ya Kikristo, kama Biblia inavyoelekeza katika **Mathayo 7:16–20**.

Katika vipimo vyote vya kutambua nabii kweli, mjumbe wa Mungu Ellen G White, alithibitishwa kuwa ni kweli ni nabii wa Mungu. Unabii wake au ujumbe alioutoa unakubariana kabisa na kweli zote za biblia, huku akiinua Biblia na kukiri kuwa Biblia ndio nuru kubwa na ujumbe aliopewa ni nuru ndogo ikituongoza kwenye nuru kubwa Biblia.

Maandiko ya Ellen G White yanamuinua Yesu kuwa ni Bwana, na kuwa alikuja duniani kama mwanadamu aliye na mwili ili aweze kumkomboa

mwanadamu. Ellen G White aliishi maisha yaliyokuwa kielelezo kwa jamii kama Biblia inavyosema kwa matunda yao mtawatambua. Zaidi ya hayo unabii alioutoa ulikuwa ukitimia kama ilivyokuwa kwa manabii wengine. Ellen G White alikuwa akipewa njozi na kuwa katika hali waliyokuwa nayo manabii wengine ndani ya biblia.

Hitimisho: Biblia inatufundisha kwamba karama ya unabii ni zawadi ya Mungu kwa Kanisa lake linaloishi katika siku za mwisho. Mtu anayesema ana karama ya unabii hapaswi kuaminiwa kwa madai yake pekee, bali lazima apimwe kwa viwango vilivyowekwa na Neno la Mungu.

Unabii ni kama taa inayotuangazia kusafiri salama katika giza nene la usiku katika siku za mwisho. 2 Petro 1:19 Nasi tuna lile neno la unabii lililo imara zaidi, ambalo, mkiliangalia, kama taa ing'aayo mahali penye giza, mwafanya vyema, mpaka kutakapopambazuka, na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu. Kanisa linaamini kwamba huduma hiyo haikupewa kuchukua nafasi ya Biblia, bali kuwaelekeza

MAMBO YA KUOMBEA: Tuwaombee watu waliorudi nyuma, **MUNGU** awarudishe kwenye kanisa lake. Wengi wamekumbana na changamoto au majaribu yaliyowafanya wajitenge na ushirika wa kiroho. Ni wajibu wetu kuwaombea kwa upendo ili Mungu awape neema ya kutubu na kurejea nyumbani kwa furaha. **Mhudumu / Kanisa laweza kuongeza mambo mengine ya kuombea katika nafasi hii.**

Somo La Sita

KAZI NA FAIDA YA KIPAWA CHA UNABII.

Na Pr. Elias Joseph Misungwi

Mkurugenzi wa Huduma Uchapishaji na Roho ya Unabii Union ya kusini mwa Tanzania

Fungu kuu: **2 Timotheo 3:16-17**- *Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika baki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*

Utangulizi: Mojawapo ya karama zinazotolewa na Roho Mtakatifu kwa kanisa lake ni karama ya unabii. Tamko rasmi la la kanisa juu ya msingi huu wa Imani inasema: “Karama hii ni alama inayolitambulisha kanisa la Masalio na ilidhihirika katika huduma ya Ellen G. White. Kama mjumbe wa Bwana, maandishi yake yanaendelea kuwa chanzo madhubuti cha ukweli yanayotoa kwa kanisa faraja, uongozi, mafundisho, na maonyo. Pia yanaweka wazi kwamba Biblia ndiyo kanuni ambayo kwayo mafundisho yote na uzoefu lazima vipimwe.” (Yoe. 2:28, 29; Mdo. 2: 14-21, Ebr. 1: 13; Ufu. 12:17; Uf. 19:10)

Mungu alitoa kipawa cha Roho ya unabii ndani ya kanisa lake kwa kazi maalumu. Kwa hiyo kipawa cha karama ya unabii kama Roho mtakatifu alivyowaongoza manabii kuandika kina faida zifuatazo kwa kanisa:

1. Kusaidia Kuanzisha Kanisa:

Kanisa limejengwa kwa msingi wa mitume na manabii, Yesu Kristo akiwa jiwe kuu la pembeni (Efe.2:20, 21).

2. Husaidia katika kuanzisha Utume wa Kanisa:

Ni kwa njia ya manabii, Roho Mtakatifu aliwachagua Paulo na Barnaba kwa safari yao ya kwanza ya kiutume (Mdo. 13:1, 2) na akaelekeza ni wapi waende kufanya kazi (Mdo.16:6-10)

3. Husaidia kulijenga kanisa kiroho:

Lakini anayetoa unabii anasema na watu akiwajenga, kuwatia moyo na kuwafaraji (1Kor.14:3). Pamoja na karama zingine za roho, unabii umetolewa kusudi la kuwakamilisha watakatifu kwa ajili ya kazi za huduma, ili kwamba mwili wa Kristo upate kujengwa. (Efe.4:12)

4. Waliunganisha na kulilinda kanisa:

Manabii walisaidia umoja wa imani na kulilinda na mafundisho ya uwongo mpaka sote tutakapoufikia umoja katika imani na katika kumjua sana Mwana wa Mungu na kuwa watu wazima kwa kufikia kipimo cha ukamilifu wa Kristo. Ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwatupwa huku na huku na kuchukuliwa na kila upepo wa mafundisho kwa hila za watu, kwa ujanja, kwa kufuata njia zao za udanganyifu. (Efe.4:13, 14)

Kwa hiyo ukikuta nabii yeyete anatoa unabii au mafundisho ya kulitawanya kanisa au kulishambulia kanisa basi huyo roho anayemwomgoza siyo roho wa Mungu. Maana roho ya manabii huwatii manabii. Nabii mwenye unabii wa kweli hana budi kulinda umoja wa mwili wa Kristo. Kwa Lugha ingine Nabii hana majivuno, anatanguliza wengine, hujishusha. Nabii au mtume wa kweli hilitambua na kulithamini Kanisa. Waefeso 3:1-13

Aya hii inathibitisha kuwa nabii au mtume yeyote hana budi: Kuwa wakili wa neema za Mungu –fungu la 2, atambue kuwa kuna manabii wengine siyo yeye peke yake, amkiri Ubwana wa Yesu Kristo, ajishushe- fungu la 8, atambue uongozi wa Mungu kupitia kanisa –fungu la 10

5. Walionya juu ya hatari zijazo:

Manabii walionya kanisa, jamii na taifa kwa ujumla. kwa mfano; Nabii mmoja katika Agano Jipya alionya juu ya njaa itakayokumba watu karibuni (Mdo.11:27-30) na wengine walionya kwamba Paulo atakamatwa na kufungwa Yerusalemu (Mdo. 20:23, 21:4, 10-14)

6. Walithibitisha imani wakati wa ushindani.

Baada ya baraza la kanisa kuamua juu ya hoja za wokovu wa mataifa mengine, manabii walitumwa kwenda kuimarisha waumini. “Yuda na Sila, ambao wenyewe walikuwa manabii wakanena maneno mengi ya kuwatia moyo na kuwajenga katika imani wale ndugu walioamini.” (Mdo. 15:32)

Kwa hiyo mtu yeyote akipata mafunuo mapya au mafundisho mapya kutoka kwa Bwana ni lazima mafundisho yake au unabii wake ulenge kulijenga kanisa ili lizidi kuwa na umoja kama lilivyokuwa ombi la Yesu kwa kwa Baba yake Yohana 17:21. Hapaswi kujitenga na mwili wa Kristo, na badala yake anapaswa kujishusha/kujinyenyekeza Bwana aweze kumtweza. Hata hivyo pia anatakiwa kuwa mvumilivu wakati maono, mafunuo au mafundisho yake yanapimwa na waumini wenzake kwa utaratibu uliwekwa ndani ya kanisa.

WITO: Hebu Mungu wetu atusaidie sana tuweze kuamini yote yalisemwa na manabii maana yaliandikwa ili kutuonya, kutufundisha sisi ili tuendeleo kumjua sana Mungu wetu tuwe wakamilifu ili hatimaye tuweze kuwa warithi wa uzima wa milele. Mungu anasema: “mwaminini BWANA, Mungu wenu, ndivyo mtakavyothibitika; waaminini manabii wake, ndivyo mtakavyofanikiwa” 2Nyakati 20:20b

Maswali ya Kutafakari

Je wewe ni nabii wa Uongo?

Unalitumia kwa uhalali neno la Unabii au unalitumia kukidhi utashi wako?

MAMBO YA KUOMBEA: Tuombee Taasisi ya (HHES) katika usambazaji wa Machapisho katika unioni yetu. Machapisho ya kiroho yana mchango mkubwa sana katika kufikia nyoyo za watu na kueneza ukweli wa neno la Mungu. Tunaomba ili Mungu abariki kazi za taasisi hii na kufungua milango ya usambazaji wa vitabu vyenye ujumbe wa sasa katika maeneo yote.

Mhudumu / Kanisa laweza kuongeza mambo mengine ya kuombea katika nafasi hii.

Siku ya Saba

USHINDI KATIKATI YA MKANGANYIKO YA MANABII WA UONGO

Na Elias J. Misungwi

Mkurugenzi wa Idara ya Uchapishaji na Roho ya Unabii

Union ya Kusini mwa Tanzania

2 Petro 2:1, *“Palitokea manabii wa uongo kati ya watu, na vivyo hivyo waalimu wa uongo watatokea kati yenu. Watu hao wataingiza mafundisho maharibifu na kumkana Bwana aliyewakomboa, na kwa njia hiyo watasababisha ghafla maangamizi yao wenyewe.”*

Utangulizi: Biblia inaweka bayana kuwa kama kuna kipawa cha karama ya unabii wa kweli, unaotoka kwa Mungu, basi kuna kipawa cha karama ya unabii wa uongo unaotoka kwa Baba wa uongo-shetani. Mtume Paulo katika kitabu cha 2Petro2:1 amezungumzia kutokea kwa manabii au waalimu wa mafundisho ya uongo zamani na akatahadharisha kwa hata siku za mwisho watakuwepo pia.

Mkanganyiko katika agano la kale

Mungu wetu amekuwa mwema sana kwa watu wake katika dhama zote. Amekuwa akitahadharisha watu wake wasije wakakanganyikiwa kwa sababu ya manabii wanaodai kuwa wametumwa au wamefunuliwa na Yeye kumbe siyo. Mfano katika kipindi cha Yeremia Mungu alitahadharisha watu wajiepushe na injili au mafundisho ya uongo.

Bwana anasema: *Yeremia 23:15-21, “Basi Bwana wa majeshi asema hivi, katika habari ya manabii, Tazama, nitawalisha pakanga, nitawanywesha maji ya uchungu; kwa kuwa kutoka kwa manabii hao wa Yerusalemu kukufuru kumeingia katika nchi yote. 16 Bwana wa majeshi asema hivi, Msisikilize maneno ya manabii wakivatabiria; huwafundisha ubatili; hunena maono ya moyo yao wenyewe; hayakutoka katika kinywa cha Bwana. 17 Daima huwaambia wao wanaonidharau, Bwana amesema, MTAKUWA NA AMANI; nao humwambia kila mtu aendaye kwa ukaidi wa moyo wake, Hamtapatwa na ubaya wa wote. 18 Maana, ni nani aliyesimama katika baraza la Bwana, bata akalifahamu neno lake na kulisikia? Ni nani aliyelitia moyoni neno langu, na kulisikia? 19 Tazama, tufani ya Bwana, yaani, ghadhabu yake, imetokea; ni dhoruba ya kisulisuli; itapasuka, na kuwaangukia waovu vichwani. 20 Hasira ya Bwana haitarudi, bata atakapokwisha kuyatimiza makusudi ya moyo wake; katika siku za mwisho mtalifahamu neno hili kabisa. 21 Mimi sikuwatuma manabii hao, lakini walikwenda mbio; sikusema nao, lakini walitabiri”.*

Katika agano la kale kulikuwa na manabii, waalimu wengi sana waliokuwa wakijituma wenyewe na kudai kuwa Mungu mwenyewe aliwatuma na walisababisha taharuki kubwa kwa waumini; Bwana Mungu hakunyamaza alitoa tahadhari kwa kanisa lake na kusema msiwaamini maana sijawatuma watu kama hao.

Mifano ya manabii wa uongo waliopinga kazi ya Mungu Agano la kale:

1. **Hanania:** Nabii wa uongo aliyepingana na Nabii Yeremia na kumwambia Mfalme kwamba nira ya Babeli ingevunjika kwa miaka miwili, lakini Yeremia alitabiri kifo chake na kikatimia mwaka huo huo (Yeremia 28). Yeremia 28:15 *“Kisha nabii Yeremia akamwambia nabii Hanania, Sikia sasa, Ee Hanania; Bwana hakukutuma; lakini unawatumainisha watu hawa maneno ya uongo.*
2. **Manabii wa Baali na Asera:** Wakati wa Eliya kwenye Mlima Karmeli, kulikuwa na manabii mia nne na hamsini wa Baali waliokula meza ya Yezebeli na kushindwa na moto kutoka mbinguni wa Mungu wa Israeli (1 Wafalme 18:19-20).
3. **Shemaya wa Nehelamu:** Alituma barua za kupinga huduma ya Yeremia na kuwahadaa watu wa Israeli wamwasi Mungu, akaadhibiwa kwa kukosa uzao. Jeremiah 29:24-32
4. **Ahabu mwana wa Kolaya na Zedekia mwana wa Maaseia:** Hawa walikuwa manabii waliowadanganya watu waliokuwa utumwani Babeli kwa kusema uongo na kuzini, na Yeremia alitabiri adhabu yao mikononi mwa mfalme wa Babeli (Yeremia 29:21-22).
5. **Noadia** - Nabii wa kike wa uongo aliyekuwa akijaribu kumtisha na kumkwamisha Nehemia wakati wa ujenzi wa ukuta wa Yerusalemu (Nehemia 6:14).
6. **Zedekia (mwana wa Kenaana)** - Nabii aliyefanya pembe za chuma na kumshawishi Mfalme Ahabu kupigana huko Ramoth-Gileadi dhidi ya mapenzi ya Mungu (1 Wafalme 22:11, 24).
7. **Manabii 400 wa Mfalme Ahabu** - Kundi la manabii waliompa Mfalme Ahabu ushauri wa uongo wa ushindi ili kumpendeza mfalme (1 Wafalme 22:6).
8. **Balaamu (mwana wa Beori)** - Ingawa alikuwa na kipawa cha neno, alipotoka na kushauri Waisraeli wakose kwa ajili ya tamaa ya mali na ujira, na anatajwa katika Agano Jipya kama mfano wa tabia za udanganyifu wa kinabii (Hesabu 22-24, 2 Petro 2:15)

Mkanganyiko katika agano Jipya

Katika Agano Jipya Bwana Yesu alionya juu ya waalimu na manabii wa Uongo ambao watakuja kwa Jina Lake. Mathayo:24: 8; Mathayo 24:23-24. Hatari kubwa iliyopo katika siku hizi za mwisho ni Kunyanyuka kwa jopo kubwa la Manabii wa Uongo. Sasa Biblia inapotaja uwepo wa manabii wa uongo, haimaanishi tu manabii bali hata waalimu, waponyaji, wahubiri, wainjilisti, mitume, wachungaji, watumishi mashemasi nk (2Petro 2:1) **Yaani kwa ufupi kila karama ina waongo wake.** Sasa watumishi wote hao wa uongo biblia imewapa jina moja la ujumla ambalo ndio hilo MANABII WA UONGO.

Mifano wa manabii wa uongo walisababisha mkanganyiko katika agano jipya:

1. **Fileto (au Figelo)** – Huyu anaitajwa pamoja na Hermogene kama watu waliomwacha Paulo na kuacha mafundisho ya kweli huko Asia (2 Timotheo 1:15).
2. **Bar-Yesu (Elimasi)** – Mchawi na nabii wa uongo wa Kiyahudi aliyempinga Mtume Paulo huko Pafo (Matendo 13:6-8).
3. **Himenayo** – Alitajwa na Paulo kama mtu aliyeacha imani na kufundisha mafundisho ya uongo kuwa ufufuo umekwisha kupita (2 Timotheo 2:17-18).
4. **Fileto** – Alishirikiana na Himenayo kueneza mafundisho hayo ya uongo yaliyoharibu imani ya baadhi ya watu (2 Timotheo 2:17-18).
5. **Aleksanda**: Mtu huyu alitajwa pamoja na Himenayo kama mtu aliyekana imani na kumwasi Mungu (1 Timotheo 1:19-20). Mtu aliyemwasi Paulo na kupinga maneno yake kwa nguvu zote (2 Timotheo 4:14-15).
6. **Diotrefe**: Huyu alikuwa Kiongozi wa kanisa aliyetajwa na Yohana kwa kupenda ukubwa, kukataa mamlaka ya mitume, na kueneza maneno mabaya (3 Yohana 1:9-10).
7. **Simoni Mchawi**: Huyu naye alitaka kununua nguvu ya Roho Mtakatifu kwa fedha na alileta fikra potofu kwenye kanisa changu (Matendo 8:9-24).

2Timotheo 3:13 “*Lakini watu wabaya na wadanganyaji wataendelea, na kuzidi kuwa waovu, wakidanganya na kudanganyika*”.

2Wathesalonike 2:10 “*na katika madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea; kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa. 11 Kwa hiyo Mungu anavotea nguvu ya upotevu, wauamini uongo; 12 ili wabukuminwe wote ambao hawakuamini kweli, bali walikuwa wakijifurabisha katika udhalimu*”.

Ndugu yangu! Hao ni manabii wa Uongo, walioruhusiwa watokee siku hizi za mwisho. wanafanya kazi yao ya kupotosha ulimwengu mzima na wakishamaliza wataenda kuhukumiwa. Manabii wa uongo walisababisha mkanganganyiko mkubwa sana katika kanisa la Mungu kipindi cha agano la kale na hata katika kipindi cha Agano jipya pia. Lakini pamoja na nguvu mbili hizo zinazopingana nguvu za mafundisho ya unabii wa kweli na nguvu za unabii wa uongo bado ushindi utapatikana kwa watu wanaochagua kwa wanyenyekevu na watiifu kwa mafundisho ya neno la Mungu.

Mungu anasema katika ufunuo 12: 11-12

¹⁰ *Nikasikia sauti kuu mbinguni, ikisema, Sasa kumekuwa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake; kwa maana ametupwa chini mshitaki wa ndugu zetu, yeye awashitakiye mbele za Mungu wetu, mchana na usiku.*

¹¹ *Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushubuda wao; ambao havakupenda maisha yao hata kufa.*

WITO: Pamoja na mkanganyiko mkubwa unaoletwa na manabii au waalimu waalimu wa uongo; Mungu ametuhakikishia ushindi kama tutakaa katika neno lake na yeye akakaa ndani yetu. Hebu tuchague kuwa upande wa Bwana anayeliongoza kanisa lake ili awe mshindi. Bwana anasema katika ufunuo 2:17- *Yeye aliye na sikio, na alisikie neno bili ambalo Robo anayaambia makanisa. Yeye ashindaye nitampa baadhi ya ile mana iliyofichwa, nami nitampa jive jeupe, na juu ya jive hilo limeandikwa jina jipya asilolijua mtu ila yeye anayelipokea.*

Maswali ya kutafakari

Je kanisani kwako kwaweza kuwa na manabii au waalimu wa uongo wanaoleta mkanganyiko?

Je unafahamu utaratibu unaotumika katika kanisa la Mungu kuhusiana na kupokea nuru mpya ya mafundisho kama mtu amepewa mafunuo mapya? Utamsaiadiaje asiye akaonekana nabii au mwalimu wa uongo anayetumiwa na shetani?

MAMBO YA KUOMBEA: Tuombee Ushindi dhidi ya dhambi. Vita dhidi ya majaribu na tamaa za mwili vinahitaji nguvu za kiungu ili kuweza kushinda. Tunapaswa kuomba Mungu atujaze neema na uwezo wa kusimama imara na kuishi maisha matakatifu yanayomtukuza Yeye.

Mhudumu / Kanisa laweza kuongeza mambo mengine ya kuombea katika nafasi hii.

Somo la nane

SIFA MBILI BAINIFU

(Somo maalumu kwa ajili ya Siku ya Robo ya Unabii)

Na William A. Spicer

Halimashauri Kuu ya Kanisa la Waadventista wa Sabato

Fungu kuu: *“Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake kupigana vita na wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushubuda wa Yesu Kristo” (Ufunuo 12:17).*

Mnamo mwaka wa 1884, mmoja wa wafanyakazi wetu, akiwa safarini kwa treni katika Jimbo la Magharibi, alianza mazungumzo na askofu wa mojawapo ya makanisa makubwa, pamoja na mhariri wa gazeti ambaye walikuwa wakisafiri naye. Mwishoni mwa mazungumzo hayo, askofu alimwambia rafiki yake mhariri: “Waadventista wa Sabato ni ajabu kubwa zaidi ya maendeleo katika kipindi cha miaka arobaini iliyopita. Licha ya upinzani wote unaoweza kuwaziwa, mafundisho yasiyopendwa na wengi, na changamoto zote, watu hawa wameinuka kutoka hali ya kutokuwa na kitu na umaskini na kuwa miongoni mwa waliofanikiwa zaidi katika kujitambulisha na kuleta athari duniani kote; na kazi yao inaendelea kusonga mbele licha ya kila kitu” (Review and Herald, Desemba 9, 1884).

Hata hivyo, mwaka wa 1884 kazi yetu ilikuwa ndiyo kwanza inaanza kuelekeza macho yake kwenye ulimwengu mpana. Wakati huo, hatukuwa na kazi yoyote nje ya Amerika Kaskazini na Ulaya. Lakini kiongozi huyu mwenye uwezo wa kutambua mambo aliona kuwa vuguvugu hilo lilikuwa na sifa za ukuaji imara na wenye mafanikio. Nakumbuka miaka kadhaa baadaye, maafisa wawili wa kanisa jingine walifika katika ofisi yetu ya Mkutano Mkuu (General Conference) huko Washington ili kupata taarifa na nyenzo za kujifunza kuhusu mpango wetu wa kazi na mfumo wa shirika; waliona kuwa mfumo huo uliwapa watu hawa wachache ufanisi wa kipekee katika utumishi, ufanisi unaozidi ule wa kawaida.

Tunajua vyema kwamba nguvu na ufanisi havimo katika mpango wowote unaoweza kuandikwa kwenye karatasi. Matokeo hutokana na kuhubiri ujumbe wa “injili ya milele,” ambayo nabii Yohana, katika kitabu cha Ufunuo, aliona ikipelekwa kwa mataifa yote wakati saa ya hukumu ya Mungu ilipowadia.

Injili hiyo bado ni “nguvu ya Mungu kwa ajili ya wokovu wa kila aaminiye” (Warumi 1:16). Lakini pamoja na kulikumbatia mfumo mkuu wa kweli za Biblia, watu wetu tangu nyakati za awali walitambua umuhimu wa huduma ya karama za kiroho ambazo Kristo aliachiwa kanisa Lake. Miongoni mwa karama hizo ilikuwa karama ya unabii, au “Roho ya unabii,” kama kitabu cha Ufunuo kinavyoita kuhusiana na kutabiri matukio ya siku za mwisho katika kazi ya injili.

Sifa kuu inayolitofautisha kanisa la vuguvugu la Ujio wa Pili, kulingana na Maandiko, ilikuwa uaminifu kwa sheria ya Mungu: “Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu na imani ya Yesu” (Ufunuo 14:12). Mara mbili, sifa hii imerekodiwa katika kitabu cha Ufunuo. Mwishoni mwa pambano kuu, Bwana anawaita watu ili kuinua tena kiwango cha sheria Yake takatifu, ambayo ule uasi mkuu ulikuwa “umewaza” kuibadilisha (Danieli 7:25).

Tangu mwaka wa 1844, wakati harakati hii mahususi ya Ujio ilipoanza, karama hii ya Roho ya Unabii ilidhihirika. Wachunguzi wa nje ya harakati hii mara nyingi wametoa ushuhuda kuhusu jinsi karama hii ya pekee ilivyokuwa na nguvu ya kujenga katika kazi ya Waadventista wa Sabato. Hata hivyo, ni wale tu walioishi na huduma ya karama hii, na kushuhudia utendaji wake wakiwa ndani, ndio wanaoweza kufahamu jinsi karama hiyo ya Roho ya Unabii ilivyokuwa na nguvu, mpya daima, thabiti, na ya uhakika katika harakati ya Ujio, kuanzia mwaka wa 1844 hadi leo. Na hivyo ndivyo itakavyokuwa daima, kwani ni karama ya kiroho ambayo huduma yake inaendelea. Kupitia jumbe zake za uvuvio, maelekezo, na shauri—zikigusia kwa kina nyanja zote za harakati hii ya mwisho ya injili—karama hii ni nguvu inayofanya kazi kwa ufanisi mkubwa katika kujenga kazi ya Mungu katika pembe zote nne za dunia.

Sifa kuu inayotofautisha kanisa la harakati ya Ujio, kulingana na Maandiko, ilikuwa ni uaminifu kwa sheria ya Mungu. “Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu” (Ufunuo 14:12). Mara mbili, sifa hii imerekodiwa katika kitabu cha Ufunuo. Mwishoni mwa pambano kuu, Bwana anawaita watu ili kuinua tena kiwango cha sheria yake takatifu, ambayo ule uasi mkuu ulikuwa “umewaza” kuibadilisha (Danieli 7:25).

Vita vya Shetani Dhidi ya Harakati Hii

Maono ya Patmo yanaonyesha zaidi ghadhabu ya Shetani dhidi ya harakati hii inayowaita wanaume na wanawake kurejea katika uaminifu kwa amri za

Mungu. Katika sura ya kumi na mbili ya Ufunuo, kanisa la nyakati zote linafananishwa na mwanamke aliyevikwa jua; ambaye Shetani amepigana naye, kwanza kupitia Roma ya kipagani katika karne za awali, kisha kupitia Roma ya kipapa katika kipindi chote kirefu cha kinabii cha miaka 1260, kikifikia “wakati wa mwisho.” Na sasa, wakati kanisa la mwisho, au “masalio,” linapopeleka ujumbe maalum wa mwisho wa injili, adui wa kweli anachochewa kuonyesha upinzani wa pekee: “Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake kufanya vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu Kristo” (Ufunuo 12:17).

Hii hapa ni sifa nyingine bainifu. Kanisa la mabaki, yaani watu wa vuguvugu la Ujio (Advent movement), walipaswa kuzishika amri, kama lilivyofanya kanisa la Agano Jipya, na walipaswa kuwa na karama ya Roho ya unabii moja ya karama hizo zilizotolewa kwa kanisa la Agano Jipya. Kwani malaika anafafanua hasa neno hili, “ushuhuda wa Yesu,” kama lilivyotumika katika unabii huo: “Ushuhuda wa Yesu ni Roho ya unabii” (Ufunuo 19:10).

Roho ya unabii ndiyo karama ambayo kwayo manabii walinena nyakati za kale. “Manabii,” anasema Petro, “walitafuta-tafuta kwa bidii” ili kujua “ni wakati gani, au namna gani ya wakati, ambao Roho ya Kristo iliyokuwa ndani yao ilikuwa ikionyesha, iliposhuhudia mapema juu ya mateso ya Kristo na utukufu utakaofuata” (1 Petro 1:10, 11).

Roho ya Kristo ilitoa “ushuhuda” kupitia kwa manabii. Huo ulikuwa “ushuhuda wa Yesu” kupitia kwa manabii kwa kanisa la kale. Hiyo ndiyo “Roho ya unabii” ambayo Kristo aliitoa kama karama kwa kanisa la Agano Jipya—“wengine mitume; na wengine manabii.” Na hapa, katika maono ya Ufunuo 12, inaonyeshwa kama karama iliyorejeshwa kwa kanisa la mabaki. Vuguvugu la Ujio lilipaswa kuanzishwa, kupangwa, na kuongozwa na Mungu katika kazi maalum ya ulimwenguni pote.

KAMA KATIKA SIKU ZA KALE

Mungu alipoliongoza kanisa Lake hapo zamani katika ule mwendo maalum kutoka Misri kwenda Kanaani, aliweka karama ya Roho ya unabii ndani ya mwendo huo. Ilikuwa ni nyenzo mojawapo ambayo kwayo mwendo huo ulipangwa, kufundishwa, na kuongozwa katika njia yake. “Kwa nabii Bwana aliwatoa Israeli kutoka Misri, na kwa nabii walilindwa” (Hosea 12:13). Hiyo imekuwa njia ya Mungu sikuzote. Lakini hapa tunaweza kuona kwamba mwendo huo wa kale unaonyeshwa kama kielelezo cha mwendo wa mwisho

wa injili: “Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa mifano; yakaandikwa ili kutupa sisi maonyo, ambao miisho ya dunia imetufikia” (1 Wakorintho 10:11).

Katika mwendo huo wa kwanza, Bwana aliweka karama ya Roho ya unabii ndani ya “kanisa Lake lililokuwa jangwani.” Katika utimilifu wa wakati wa unabii, mwendo wa Ujio ulitokea. Sasa Bwana “ameunyosha mkono wake tena mara ya pili ili kuwakomboa mabaki ya watu wake... kutoka pembe nne za dunia” (Isaya 11:11, 12). Na mwendo huu wa mwisho ulipoinuka, Bwana alikusudia kulipa kanisa Lake tena karama ya Roho ya unabii.

Hii Inamaanisha Nini?

Wapinzani wa wazo lolote la kudhihirika tena kwa karama hiyo wamesisitiza kuwa neno “kutoa unabii” wakati mwingine lilimaanisha kutoa ushuhuda tu, kama vile kumshuhudia Kristo mbele ya wanadamu. Lakini hakuna nafasi hapa kwa tafsiri hiyo. Unabii hapa unazungumzia alama mbili bainifu za kanisa la mwisho. Linadumisha kitu fulani, na lina au linamiliki kitu fulani. Linadumisha “amri za Mungu,” na lina “ushuhuda wa Yesu.” Hilo la pili si jambo ambalo kanisa hulifanya, kama nyongeza ya kushika amri; ni kitu ambacho “linacho” au kilicho mikononi mwake. Lilipaswa kuwa na karama ya Roho wa unabii ndani yake. Ni kitu cha kumiliki na kushikilia. Yohana alipokaribia kuanguka miguuni pa malaika, katika maono yake, ili kuonyesha heshima, malaika alimzuia akisema, “Angalia usifanye hivyo. Mimi ni mtumishi mwenzako na wa ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu: mwabudu Mungu: kwa maana ushuhuda wa Yesu ndio Roho wa unabii” (Ufunuo 19:10).

Tena, kwa mara ya pili, malaika alifafanua neno hilo, kana kwamba anajibu mashambulizi ambayo yangeelekezwa dhidi ya karama hii katika kanisa la mabaki lililotabiriwa. Zingatia kurudiwa kwa onyo la kumzuia Yohana katika hamu yake ya kumheshimu malaika: “Angalia usifanye hivyo; mimi ni mtumishi mwenzako na wa ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu” (Ufunuo 19:10). “Angalia usifanye hivyo: mimi ni mtumishi mwenzako na wa ndugu zako manabii” (Ufunuo 22:9). “Ushuhuda wa Yesu,” kama neno hilo linavyotumiwa mahususi hapa, “ndio Roho wa unabii,” na huyu ndiye Roho aliyewatendea kazi ndugu zake Yohana, yaani “manabii.”

Picha kamili ya unabii huu iko wazi. Katika siku za mwisho, wakati kazi ya hukumu ya kuhitimisha ilipoanza mbinguni, harakati maalum ya ujio ilipaswa kutokea duniani; kupitia harakati hiyo, ujumbe mkuu wa sehemu tatu wa Ufunuo 14 ungepelekwa kwa kila taifa, lugha, na watu.

Sifa Mbili Bainifu Huenda Pamoja

Kama tulivyoona, kulikuwa na sifa mbili maalum ambazo zingetofautisha kanisa hili la “masalio” la harakati hiyo. Kama ilivyokuwa kwa kanisa la Agano Jipya, walipaswa “kuzishika amri za Mungu na imani ya Yesu,” na vilevile, kama kanisa la Agano Jipya, walipaswa kuwa na “Roho ya unabii” katikati yao. Inafaa kwamba kanisa ambalo limekabidhiwa upya kazi ya kuinua sheria ya Mungu iliyodharauliwa, lipokee pia urejesho wa karama ya unabii. Sheria takatifu na karama ya unabii zinahusishwa pamoja katika Maandiko: “Pasipo maono watu huangamia; bali yeye aishikaye sheria ana heri” (Mithali 29:18); “Sheria haipo tena; manabii wake pia hawapati maono kutoka kwa Bwana” (Maombolezo 2:9). Katika “kuacha imani” kukubwa kulikotokea baada ya siku za mitume, sheria ya Mungu na kweli ya Mungu zilikanyagwa chini ya miguu. Pamoja na kurejeshwa kwa ujumbe kamili wa amri za Mungu, unabii unaonyesha pia kurejeshwa kwa maono ya kinabii.

Waanzilishi wa harakati ya ujio walielezea vyema urejesho huu wa karama katika utangulizi wa sehemu ya pili ya kitabu “Early Writings” (Maandiko ya Awali), mojawapo ya vitabu vya kwanza kabisa vya harakati ya ujio:

“Karama ya unabii ilidhihirika katika kanisa wakati wa kipindi cha Wayahudi. Ikiwa ilitoweka kwa karne kadhaa, kutokana na hali ya uharibifu wa kanisa kuelekea mwisho wa kipindi hicho, ilijitokeza tena mwishoni mwake ili kutangaza kuja kwa Masihi. Zekaria, baba yake Yohana Mbatizaji, ‘alijazwa Roho Mtakatifu, akatoa unabii.’ Simeoni, mtu mwenye haki na mcha Mungu ambaye ‘alikuwa akingojea kufarijiwa kwa Israeli,’ aliongozwa na Roho kuingia hekaluni, akatoa unabii kumhusu Yesu kama ‘nuru ya kuwaangazia Mataifa, na utukufu wa Israeli,’ na Ana, nabii wa kike, ‘alinena habari Zake kwa wale wote waliokuwa wakitazamia ukombozi Yerusalemu.’ Na hakukuwa na nabii mkuu kuliko Yohana Mbatizaji, ambaye alichaguliwa na Mungu kumtambulisha kwa Israeli ‘Mwana-Kondoo wa Mungu aondoaye dhambi ya ulimwengu.’

“Enzi ya Ukristo ilianza kwa kumiminwa kwa Roho, na aina mbalimbali za karama za kiroho zilionekana miongoni mwa waamini. . . .Tangu wakati wa uasi mkuu wa imani, karama hizi zimeonekana mara chache sana; na hii labda ndiyo sababu inayowafanya Wakristo wengi kuamini kuwa zilikuwa za kipindi cha kanisa la awali pekee. Lakini je, si kwa sababu ya makosa na kutokuamini kwa kanisa ndiyo maana karama hizo zimekoma? . . . Na kwa kuwa kazi maalum ya Roho ilihitajika ili kuandaa watu kwa ajili ya kuja kwa mara ya kwanza kwa Kristo, ni kwa kiasi gani zaidi inahitajika kwa ajili ya

kuja Kwake kwa mara ya pili! Agizo la mitume lilihusu enzi ya Ukristo, na liliijumuisha yote. Hivyo, karama hizo zilipotea kwa sababu ya uasi wa imani tu, na zitafufuliwa pamoja na kufufuliwa kwa imani na matendo ya kanisa la awali.”Early Writings, uk. 133-135.

Na pamoja na kufufuliwa kwa imani ya awali—“amri za Mungu, na imani ya Yesu”—karama ya Roho wa unabii ilijitokeza tena, kama ilivyotabiriwa katika maono ya Yohana kwenye Kisiwa cha Patmo.

Kalamu ya Unabii Ilichukuliwa Tena Mwaka 1844

Zamani za kale, nabii aliyekuwa Patmo aliandika kuhusu utukufu wa Kurudi kwa Bwana mara ya pili, kama alivyokuwa ameona katika maono. Alieleza kuhusu Yerusalemu Mpya. “Mimi Yohana niliona mji mtakatifu,” aliandika (Ufunuo 12:2). “Niliona mbingu mpya na nchi mpya” (Ufunuo 21:1). Aliona kuibuka kwa vuguvugu la injili duniani kote, wakati saa ya hukumu ya Mungu ilipowadia. Aliwaona watu wakijitokeza mwaka 1844, wakishika amri za Mungu. Pamoja na kuibuka kwa vuguvugu hilo, aliona karama ya Roho ya unabii ikirejeshwa katika kanisa la mabaki. Mtume na nabii huyo mzee aliandika mambo hayo na kuweka chini kalamu ya Ufunuo. Karne kumi na tisa baadaye, mwaka 1844, kijana mmoja aliyekuwa sehemu ya vuguvugu la Ujio (Advent movement) alichukua kalamu ya unabii, na kuanza kuandika kuhusu maono ya utukufu wa kuja kwa Kristo, Yerusalemu Mpya, na nchi ya mbinguni—mambo yaleyale ambayo nabii wa Patmo aliyaandika, lakini sasa yakionyeshwa kama utukufu utakaofunuliwa hivi karibuni. Hakukuwa na kushindwa kwa unabii wa kitabu cha Ufunuo. Wakati ulikuwa umewadia, watu wa unabii walijitokeza, nao walikuwa na karama iliyotabiriwa.

MWISHO: Mhudumu atoe wito kwa washiriki wote kununua, kusoma, na kuishi ukweli wa vitabu vya Mama Ellen G. White, kwa kuwa machapisho haya ni urithi mtakatifu kutoka kwa Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi. Kisha, wawe tayari kushiriki kweli hizi na watu wengine ili wote waweze kubarikiwa.

Baada ya hapo, mhudumu aongoze ombi la shukrani kwa Mungu kwa baraka kuu ya uwepo wa Roho ya Unabii katika kanisa, akiomba Bwana awabariki na kuwapa washiriki wote kiu ya kusoma vitabu vya Roho ya Unabii ili wapate maarifa ya ukweli na baraka tele maishani mwao kulingana na mpango wa Bwana Mungu ambaye ndiye Mwenye ujumbe maalumu kwa ajili yao na watu wote.

Ujumbe wa somo hili umenukuliwa kutoka katika kitabu **The Spirit of Prophecy in the Advent Movement** kilichoandikwa na Mzee William A. Spicer, mhudumu na kiongozi aliyependwa sana, ambaye aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa Halmashauri kuu (General Conference) wa Waadventista Wasabato kuanzia mwaka 1903 hadi 1922, na baadaye Mwenyekiti kuanzia mwaka 1922 hadi 1930. Kujitolea kwa Mzee Spicer katika kazi ya misheni na uaminifu wake katika kusimamia kazi ya Mungu kunakumbukwa milele kupitia kauli yake maarufu kuhusu maana ya kumtumikia Mungu: “Hakuna vyeo vya heshima, bali kuna vyeo vya utumishi pekee” (Iliandikwa kutoka San Francisco, California, tarehe 22 Mei, 1922).